## 4.2 Madhara ya kiuchumi yatokanayo na chakula kilichochafuliwa na viuatilifu

Madhara ya kiuchumi yanaweza kutokea kwa mkulima na nchi kwa ujumla. Mkulima anaathirika kiuchumi kutokana na usugu wa visumbufu vya mimea hivyo kusababisha ongezeko la gharama. Pia mazao kutokubalika katika soko la ndani na nje ya nchi kutokana na mabaki ya viuatilifu kwenye chakula. Athari nyingine ni kuongezeka kwa gharama za udhibiti.

## 5. Udhibiti wa mabaki ya viuatilifu katika chakula

Udhibiti wa mabaki ya viuatilifu katika chakula ni muhimu kuzingatiwa katika mnyororo wa thamani kuanzia shambani, uhifadhi na usambazaji wa mazao kwa kuwa mlaji wa mwisho ni vigumu kudhibiti au kutambua uwepo wa mabaki hayo.

Ni muhimu kwa mkulima, mhifadhi na msambazaji wa mazao kuhakikisha mabaki ya viuatilifu kwenye mazao hayazidi kikomo salama kwa kuzingatia yafuatayo: -

- Kufuata ushauri wa kitaalam katika matumizi sahihi ya viuatilifu,
- Utumiaji wa viuatilifu uzingatie maelekezo yaliyoandikwa kwenye lebo,
- Kuzingatia muda wa kuisha viuatilifu katika mazao (postharvest interval)
- Kuweka kumbukumbu za matumizi ya viuatilifu.
- Kuepuka utupaji holela wa viuatilifu unaoweza kupelekea uchafuzi wa mazingira na kuathiri mimea

*Kumbuka*: *Uelewa juu ya athari za kiafya na kiuchumi kwa kila mmoja katika mnyororo wa thamani kutachangia kupunguza na kuondokana na madhara ya mabaki ya viuatilifu katika chakula.*

## 6. Hitimisho

Udhibiti wa mabaki ya viuatilifu kwenye mazao ya chakula ni muhimu katika kuchangia upatikanaji wa chakula salama nchini. Matumizi sahihi ya viuatilifu yanapaswa kuzingatia ushauri wa wataalam ikiwa ni pamoja maelekezo yaliyoandikwa kwenye lebo/ vifungashio.

## Kwa maelezo zaidi, wasiliana nasi kwa anwani zifuatazo:


**MKURUGENZI MKUU**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
S.L.P. 9524, Dar es salaam
Hotline: + 0800 110 827/ Nukushi: + 255 22 2450959
Baruapepe: info@tbs.go.tz/ Tovuti: www.tbs.go.tz
Malalamiko: malalamiko@tbs.go.tz

**OFISI ZA KANDA:**
**NYANDA ZA JUU KUSINI**
(Iringa,Mbeya, Njombe and Songwe)
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S.L.P.1674 Mbeya, Tanzania
Simu: 025 2502848/ Nukushi: 025 2502848

**KANDA YA ZIWA**
(Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simyu and Shinyanga)
Jengo la NSSF ,Ghorofa ya 3
S.L.P.1814 Mwanza, Tanzania
Simu: 028 2505044/ Nukushi: 028 2505044

**KANDA YA KASKAZINI**
(Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga)
Ngorongoro Tourist Center, Ghorofa ya 6
S.L.P.2399 Arusha,Tanzania
Simu: 027 2520143 / Nukushi: 027 2520143

**KANDA YA KATI**
(Dodoma, Singinda, and Tabora)
Kambarage Tower, Ghorofa ya 6
S.L.P.2956, Dodoma,Tanzania
Simu: 026 2320310 / Nukushi: 0262320310

**KANDA YA KUSINI**
(Lindi, Mtwara, and Ruvuma)
Jengo la PSSSF, Sokoine House, Ghorofa ya 3
S.L.P.1396 Mtwara, Tanzania
Simu: 023 2334477 / Nukushi: 023 2334477

**KANDA YA MAGHARIBI**
(Katavi, Kigoma, and Rukwa)
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S.L.P.1276 Kigoma,Tanzania
Simu: 028 2804023/ / Nukushi: 028 2804023

**KANDA YA MASHARIKI**
(Dar es, Salaam, Morogoro na Pwani )
Jengo la PSSSF (Commerical Complex) Ghorofa ya 4
S.L.P.9425, Dar es Salaam

TBS_Tanzania tbs_viwango Tbs_viwango TBS Viwango TV


TANZANIA BUREAU OF STANDARDS
tbs

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)

# UDHIBITI WA MABAKI YA VIUATILIFU KATIKA CHAKULA

# 1. UTANGULIZI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni shirika la umma lililo chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambalo linatekeleza majukumu yake kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Viwango, Sura 130. Moja ya majukumu hayo ni kusimamia masuala ya chakula salama ili kulinda afya ya jamii na kuwezesha biashara.

Chakula kinachotokana na mazao ya kilimo kinatakiwa kuwa salama mlaji. Wakulima hutumia viuatililifu katika kuua, kufukuza au kudhibiti visumbufu vya mimea. Zipo aina mbalimbali za viuatilifu ambazo hugawanywa kutegemeana na kisumbufu lengwa (target organism), asili ya kiuatilifu (origin) na umbo la kikemikali (chemical structure). Hata hivyo, viuatilifu visipotumika kwa usahihi vinapelekea kufanya chakula husika kutokuwa salama.






## 2. Mabaki ya viuatilifu katika mazao ya chakula

Matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu kwenye mazao husababisha uzalishwaji wa mazao yenye mabaki ya viuatilifu kwenye mnyororo mzima wa thamani. Mabaki ya viuatilifu yanapozidi kikomo salama kwa mlaji (Maximum Residue Limit – MRLs) hupelekea chakula hicho kutokuwa salama. Vikomo salama vya mabaki ya viuatilifu kwenye mazao huwekwa kimataifa kupitia kamati ya kitaalamu ya Codex Alimentarius Commission iliyo chini ya Shirika la Afya Duniani na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (WHO/FAO) na kuasiliwa na TBS kuwa viwango vya kitaifa.

## 3. Visababishi vya mabaki ya viuatilifu katika chakula

Kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya viuatilifu katika uzalishaji wa mazao mbalimbali hususani sekta ya mbogamboga na matunda. Aidha, ongezeko hili limechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo suala la mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamepelekea kuongezeka kwa visumbufu vya mazao vinavyoshambulia mimea.

**Hali hii imeambatana na matumizi ya viuatilifu bila kuzingatia yafuatayo: -**

- Kutozingatia muda unaoshauriwa kabla ya kuvuna mazao yaliyowekewa viuatilifu;
- Kutokufuata maelezo ya matumizi ya viuatilifu kama yalivyoainishwa kwenye lebo (matumizi ya viuatilifu kwa kiasi tofauti na ilivyoelekezwa, au kwa mimea ambayo haijashauriwa);
- Matumizi mabaya ya vifungashio vilivyotumika kuwekea viuatilifu;
- Matumizi ya viuatilifu kwa kiasi kikubwa kuliko kinachoshauriwa na wataalamu;
- Matumizi sahihi ya viuatilifu kwa mazao yaliyo tayari kuvunwa au mazao yaliyokwisha vunwa;
- Matumizi ya vifaa vilivyochafuliwa na viuatilifu (kutokuosha vifaa vinavyo tumika kuchanganyia au kuhifadhia, kupimia, au makosa wakati wa kuchanganya viuatilifu);
- Uwekaji holela wa viuatilifu, unaoweza kusababisha uchafuzi wa mazao
- Kutumia viuatilifu bila kushauriwa na mtaalamu wa kilimo
- Matumizi ya viuatilifu zisizoruhusiwa na Mamlaka husika
- Uchanganyaji wa viuatilifu mbalimbali bila kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo ili kuharakisha ukuaji wa mimea au kuua visumbufu vya mimea kwa haraka
- Kutokuzingatia kanuni bora za kilimo;

## 4. Athari zitokanazo na uwepo wa mabaki ya viuatilifu katika chakula

Viuatilifu ni muhimu katika kuzuia mimea isishambuliwe na visumbufu vinavyochangia uharibifu na magonjwa ya mimea. Matumizi yasiyo sahihi yanasababisha madhara ya kiafya na kiuchumi kwa jamii.

Kumbuka: *Mabaki ya viuatilifu kwenye mazao kwa kikomo kisicho salama husababisha madhara ya kiafya, ambayo huweza kujitokeza baada ya muda mfupi au muda mrefu.*

### 4.1 Madhara ya kiafya yatokanayo na kula chakula kilichochafuliwa na viuatilifu

Viuatilifu vikitumika bila kuzingatia kanuni bora za kilimo huweza kusababisha madhara ya kiafya kwa mlaji wa chakula. Madhara hayo huweza kujitokeza baada ya muda mfupi au mrefu kutegemea;

- kiasi cha mabaki ya viuatilifu kwenye chakula,
- muda ambao chakula chenye mabaki kimekuwa kikitumika,
- umri wa mlaji
- hali ya afya ya mlaji kwa ujumla.

Kumbuka: *Mtumiaji wa viuatilifu asipotumia ipasavyo vifaa vya kujikinga anaweza kuvuta hewa yenye viuatilifu, kuathirika ngozi na macho na kupelekea madhara ya kiafya.*

#### 4.1.1 Madhara ya muda mfupi

Haya ni madhara ya kiafya yanayotokana na kula chakula chenye mabaki ya viuatilifu kwa kiasi kikubwa ndani ya muda mfupi. Dalili zake ni maumivu ya tumbo, kizunguzungu, maumivu ya kichwa, kutapika, kukosa hewa, kukohoa na kuwepo kwa matatizo ya ngozi na macho.

#### 4.1.2 Madhara ya muda mrefu

Haya ni madhara ya kiafya yanayotokana kula chakula chenye mabaki ya viuatilifu kwa kiasi kidogo kwa muda mrefu. Madhara hayo ni kama vile kupata saratani, athari ya kingamwili, kupata msongo wa mawazo na kupata matatizo ya mfumo wa fahamu.